TOLEO NO.80

Khilafah

JAMADUL AWWAL 1448 HIJIRIA - NOVEMBA 2026 MILADIA (Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

UBEPARI WACHOCHEA WATU KUJIUA



Takwimu zinaonesha kwamba takriban watu 720,000 hujiua kila mwaka, na zaidi ya idadi hii hufanya majaribio ya kujiua. Asilimia 73% ya kujitoa uhai hutokea katika nchi za uchumi wa chini na wakati kati ya vijana wa umri wa miaka 15 -29.

Vichocheo vya kujia ni vingi vikiwemo vya mazingira, jinsi, baiolojia na kijamii. https://www.who.int/news-room/fact-sheets/detail/suicide#:~:text=More%20than%20720%20000%20people,cause%20of%20death%20among%2015%E2%80%9329%2Dyear%2Dolds.

Uhai na thamani yake ni suala la kimaumbile lisilokuwa na mbadala kwa mwanadamu. Basi huwa ni jukumu kuu la serikali yoyote makini kulinda na kuhifadhi uhai wa watu wake, kuzuiya matukio ya kujiua na kuboresha maisha ya watu.

Utofauti wa mifumo ya kimaisha inayotawala maisha ya watu huwa na athari kubwa katika kulinda na kuhifadhi uhai wa watu.

Mfumo wa ubepari unaotawala dunia leo hii umeifanya dunia kuwa mahali hatari sana kimaisha kiasi cha kwamba wengi wa watu huona uhai hauna tena maana.

Ugumu wa maisha kutokakana na kipato duni kwa sababu ya sera thakili za kiuchumi za ubepari, gharama za maisha kuwa juu kiasi watu kushindwa kupata mahitaji yao, serikali kuwa mzigo badala ya kuwa mtoa suluhisho kwa maisha ya watu kwa kuweka makodi na malipo kwa kila huduma ikiwemo afya na usalama imesababisha kuwepo kwa watu kuona maisha hayana faida yoyote na bora kuyaondoa kabisa.

Na kwa bahati mbaya kwakuwa mfumo wa kibepari hauyapi maisha fungamano na Mungu Muumba, imekuwa rahisi watu kuona kujiua ndio suluhisho. Aidha, na kwakuwa kila ...

Inaendelea ...Uk. 3

UBAGUZI WA WAGENI KAMWE HAUTOIOKOA KENYA ILIYOZINGIRWA NA UBEPARI



Karibuni serikali ya Kenya ilielekeza mamlaka zake kuchukua hatua dhidi ya raia wa kigeni wanaoendesha biashara ndogo ndogo. Agizo hii tangu hapo limeripua wasiwasi kuhusu Ubaguzi wa Wageni na kuzua hofu kubwa kuhusu unyanyasaji, uonevu, na uhamishaji wa kinguvu kwa wageni hususan raia wa Burundi nchini Kenya.

Tatizo la Chuki kwa Wageni ni matokeo ya fikra ya 'aswabia' fikra ambayo watu wa mahali fulani hujiona bora kuliko wengine. Ni matokeo ya moja kwa moja ya kushindwa kwa mfumo wa urasimali (Ubepari) katika kuhudumia watu wa eneo fulani ipasavyo na badala yake hutumia wageni kama mbuzi wa kafara. Zaidi ya hayo, Urasimali umejengwa juu ya ubinafsi na maslahi pekee huku ukipuuzia mateso, iwe kutoka kwa raia wake au wageni.

Inaendelea Uk. 3

Yaliyomo :

- **Tahriri—Hakuna Urithi kwa Watoto nje ya Ndoa……2**
- **Aina za ardhi katika hukmu ya Kiislamu ……..…… 4**
- **Uzuri wa Mwanamke Kiislamu.....5**
- **Mambo gani kuchukua na kuacha kutoka kwa makafiri? ……. 7**

URITHI KWA WATOTO NJE YA NDOA: MLENGWA NI UISLAMU

Karibuni serikali kwa kuptia Naibu Waziri wa Sheria Zainabu Katimba ilitoa msisitizo kwamba itaendelea kusimamia urithi wa wanawake na watoto hata kwa watoto wa nje ya ndoa.

Kauli hii ilitolewa na Waziri-Katimba wakati alipokuwa akijibu swala la msingi la Mbunge wa Viti Maalumu Tinnar Chenge, bungeni aliyetaka kufanywe marekebisho ya Sheria ya mirathi ili mali za mama na watoto waliozaliwa nje ya ndoa zijumuishwe katika mirathi.

Pamoja na kwamba Sheria ya Mirathi na Uthibitishaji wa Wosia Tanzania kwa mujibu wa Waziri Katimba inatambua taratibu za mifumo mbalimbali ya urithi zikiwemo taratibu za kimila , kidesturi na kidini ikiwemo dini ya Kiislamu, lakini hali hiyo isiwafanye Waislamu kujipweteka na kuridhika bali jambo hili walichukuwe kwa uzito mkubwa na kuzibua vichwa vyao katika upande wa dini yao.

Kama kulivyo na kampeni kabambe ya kimataifa inayoongozwa na Marekani dhidi ya Uislamu, huku maadui wakidandia kila aina ya silaha ikiwemo kupaka matope na kushutumu sheria na hukmu mbalimbali za Kiislamu kama vazi la mwanamke, ndoa za wake wengi, vivo hivyo wanadandia suala la urithi wa Kiislamu. Na kimsingi ni Uislamu pekee ndio unaokataza kwa ukali suala la zinaa, dini na mila nyengine hazijali uovu wa zinaa wala watoto wa nje ya ndoa , Kwa hivyo, kauli za msisitizo za kutaka watoto wa nje ya ndoa wapatiwe urithi mlengwa mkuu hapo ni Uislamu na Waislamu.



Katika mfumo wa sheria za kisekula, Uislamu umepewa nafasi duni ya mila na desturi, na mara nyingi unapowasikia wanaharakati wakitaja tamko “ mila potofu’ huwa wanalenga sheria za Kiislamu.
Huu ni unyonge usio na mfano, na kimsingi ubepari hauna haja na sheria za Kiislamu hata kijipande kidogo. Ndio maana endapo Muislamu ataacha sheria yake ya Kiislamu na kwenda katika mahkama za kisekula kudai anachodhani amedhulumiwa katika sheria za Kiislamu hupokelewa kwa mikono miwili, na sheria ya Kiislamu kutupiliwa mbali. Hilo ni dalili ya kuwa uwepo wa sheria zinazoitwa za kimila ikiwemo sheria za Kiislamu ni ujanja wa maneno tu. Katika hali ya kuhuzunisha na kusikitisha ni kuona kwamba nchi changa hutenzwa nguvu na kuletewa maagizo na sheria na mataifa ya magharibi ambazo ziko kinyume na jamii zao, lakini kwa sababu ya kupatiwa misaada na hidaya za hapa na pale hunyenyekea kwao kikamilifu.

Waislamu lazima tuwe na msimamo wa kuzithamini, kuzitukuza na kuzilinda sheria zetu, kama hatukua makini kuna siku hata hicho kichache katika mambo ya ndoa na mirathi tutapokonywa kabisa na mfumo wa sheria za kisekula.

Lakini kwa upana wake kwa kuwa Uislamu ni mfumo ulioujumuisha nidhamu mbalimbali iwe sheria, uchumi, siasa nk. Basi si sawa kutosheka na baadhi ya sheria tu ambazo hata utekelezaji wake huwa haukamiliki chini ya mfumo wa kisekula.
Ni wajibu kama Umma bora kufanya kazi ya ulinganizi wa kurejesha tena maisha ya Kiislamu ili sheria zote za Kiislamu zitekelezwe kikamilifu kwa kupitia dola yake ya Khilafah inayopaswa kuanzia katika nchi kubwa za ulimwengu wa Kiislamu na kuenea mashariki na magharibi.

Mhariri

01 Jamadul Awwal 1448 Hijria

Novemba 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

Chuki dhidi ya Wageni na fikra ya utaifa uzalendo zote ni fikra za kikoloni zinazotumika kuhamasisha chuki na kugawanya watu na mataifa. Jamii ya Afrika Mashariki, licha ya mwingiliano wake wa kihistoria na tamaduni za kikabila na uhusiano wa kikoo, inaweza kusambaratishwa kwa urahisi kutokana na fikra hii ya chuki dhidi ya Wageni.

Kampeni ya kuwafukuza wageni nchini Kenya inaonesha ukweli kwamba ubepari umeibwaga chini Kenya bali umeshindwa duniani kwa ujumla. Kulingana na Ofisi ya Kitaifa ya Takwimu ya Kenya (KNBS), takriban 39.8% ya idadi ya watu wa Kenya waliishi chini ya mstari wa umaskini wa kitaifa mnamo 2022. Aidha, Kipimo cha umasikini cha Kimataifa cha Benki ya Dunia kinakadiria kuwa 43.3% ya Wakenya waliishi chini ya kiwango cha kimataifa cha dola 3 za Marekani kwa mtu mmoja kwa siku mnamo 2025. Kwa hiyo, badala ya Kenya kupambana na adui halisi ambaye ni mfumo wa Ubepari, nchi hiyo inajificha nyuma ya kampeni isiyo na tija yeyote ya kuhamasisha chuki dhidi ya Wageni.

Zaidi ya hayo, hatua hii ya Kenya ya Chuki dhidi ya Wageni inaonesha urongo wa mashirika na jumuiya za kikanda na kimataifa kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) nk.
Inaendelea uk. 6

anayekufaa mabepari huona ndiyo mwisho na hudanganyana kwamba amepumzika kwa amani, “rest in peace”, basi wengi humalizia kuamua hatima ya uongo ya kujitoa uhai.

Kubadilisha kwa kuondoa mfumo wa ubepari unaotawala ulimwengu na kuuweka mfumo wa Uislamu ndio suluhisho pekee sahihi na endelevu.

Serikali ya Kiislamu ya Khilafah imeweka msingi na kuwajengea watu ufahamu wa uwepo wa Mungu Muumba, Yeye ndie Anayemiliki uhai na mauti, na ni marufuku kujitoa uhai kiholela, kwani jambo hilo ni katika madhambi makubwa.

Aidha, Uislamu ukaja na fikra ya tiba ya kuondoa msongo wa mawazo kwa Muislamu kwa kumjenga daima awe namtegemea Mwenyezi Mungu katika mambo yake na asikate tamaa. Bali imani ya uwepo Siku ya Malipo pia inamuongezea Muislamu utulivu wa nafsi kwamba yote yanayomkuta yana mwisho na kuna hesabu. Basi Uislamu ukamtaka Muislamu ajifunge kwa uthabiti na subra wakati wa mitihani.

Bali pia kivitendo katika miamala mbali mbali Uislamu ukaondoa sababu za upweke zinazomfanya mtu kufikiria kujitoa uhai. Kwa mfano, mtu mwenye shida inapasa kusaidiwa na japo ni aibu yampasa kukopa. Pia mwenye kudaiwa anapoomba kuongezewa muda wa malipo kwa mdai, yampasa mdai akubali, na akisamehe ni bora zaidi, kwa kuwa hupata malipo makubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Pia Uislamu una ibada maalumu ya kutoa Zakat inayotoka kwa matajiri ili kusaidia masikini na wenye madeni. Hivyo, kupunguza kama siyo kuondoa fikra ya upweke ya mtu kujiona dunia imemuelemea kiasi cha kuamua kujiua.

Katika upande wa kijamii Uislamu umesisitiza ndoa na kuhimiza kufanywa nyepesi, Ukawajibisha kuwa karibu na jamaa na wazazi nk. Haya yote yanamfanya mtu kuwa mbali na fikra za kujitenga na upweke ambao hatimae hupelekea kujitoa uhai kiholela

Kwahivyo, ni wazi tukiyaangazia maisha kwa jicho la Kiislamu, kuna uwezekano mkubwa sana wa kuondoa changamoto hizi za kujitoa uhai zinazoletwa na watu kuchanganyikiwa kutokana na mfumo batil na thakili wa ubepari.

****



TOFAUTI BAINA YA KUWA SHINGO YA ARDHI NI YA MTU BINAFSI NA KUWA SHINGO YA ARDHI NI YA SERIKALI

Swali:

Swali :

Nini tofauti baina ya kuwa shingo ya ardhi na manufaa yake ni ya mtu binafsi na kuwa shingo ya ardhi ni ya serikali na lakini manufaa yake ni ya mtu binafsi?

Jawabu:

Ardhi kwa mujibu wa hukmu za kisheria ni aina mbili: ardhi ya ushr na ardhi ya kharaj, na aina zote hizi mbili ni sawa kubadilishana kwa kuuza, kununua, hiba, na hurithiwa kutoka kwa mmiliki wake, kwasababu (hiyo ardhi) ni umiliki wa kweli kwa mmiliki wake, kwa hiyo hufanyiwa kazi juu yake hukmu zote za umiliki. Na hakuna tofauti kati yao (hizo ardhi) isipokuwa katika mambo mawili tu.

La kwanza linahusiana na kitu hasa (*'ain)* anachomiliki, la pili linahusiana na lililowajibu juu ya ile ardhi.

1-Ama linalohusiana na kitu hasa (*'ain)* anachomiliki, hakika ya mmiliki wa ardhi ya 'ushr' anamiliki shingo ya ardhi na manufaa yake, na mmiliki wa ardhi ya kharaj humiliki manufaa yake tu na hamiliki shingo yake. Na hupatikana juu ya hili kuwa hukmu ya kisheria ambayo katika sharti za kusihi kwake umiliki wa kitu chenyewe hasa (*'ain)* ni kuwa mmiliki wa ardhi ya kharaj hawezi kukifanya isipokuwa mmiliki wa ardhi ya ushr.

Mfano *wakf*, sharti ya kusihi kwake ni umiliki hasa wa kitu chenyewe kinachowekwa *wakf*.



Kwa hivyo, mmiliki wa ardhi ya ushr atakapotaka kuweka *wakf* ardhi yake ambayo anaimiliki anaweza kufanya hivyo wakati wowote ule atakapo, kwasababu yeye ndie anaemiliki kitu chenyewe hasa (*'ain)*, yaani shingo yake. Lakini mmiliki wa ardhi ya kharaj atakapotaka kuweka *wakf* ardhi yake ambayo anaimiliki, huyu hawezi kufanya hivyo, kwasababu mwenye kuweka *wakf* hushurutishwa awe mmiliki wa kitu chenyewe hasa ambacho anakiweka *wakf*. Na mmiliki wa ardhi ya kharaj hamiliki ile ardhi yenyewe hasa (*'ainul-ardh)* yaani shingo yake, bali hakika yeye anamiliki manufaa yake, kwasababu shingo yake ni umiliki wa hazina ya dola (*baitul-maal*)

2-Ama linalohusiana na lililowajibu juu ya ardhi, hakika ardhi ya 'ushr' juu yake (hulipwa) 'ushr,' na ardhi ya kharaj juu yake (hulipwa) kharaj. Na tofauti kati ya ushr na kharaj ni kama ifuatavyo:

-*'Ushr'* ni fungu la kumi la kinachozalishwa na ardhi, ambapo serikali huchukua fungu hilo (*ushr*) ya kinachozalishwa kivitendo kutoka kwa mkulima wa ardhi ikiwa ile ardhi inanyeshelezewa maji kikawaida na mvua. Na ikiwa ardhi inanyeshezelewa kwa umwagiliaji au kwa njia nyengine basi (serikali) huchukua nusu ya fungu la kumi (*nisful-ushr)* katika kinachozalishwa kivitendo. Muslim amepokea kutoka kwa Jabir amesema: Kasema Mtume (SAAW):

« فِيمَا سَقَتْ الْأَنْهَارُ وَالْغَيْمُ الْعُشُورُ وَفِيمَا سُقِيَ بِالسَّانِيَةِ نِصْفُ الْعُشْرِ»

"Kwa kinachonyweshelezewa na mito na mawingu (mvua) hutolewa fungu la kumi, na kinachonyweshelezewa kwa umwagiliaji hutolewa nusu ya fungu la kumi".

Na *'ushr'* hii huzingatiwa kuwa ndio zaka, na huwekwa katika hazina (*baitul-maal)*, na haitumiwi isipokuwa kwa ajili ya mbeya/aina katika zile mbeya nane zilizotajwa katika Aya:

﴿إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾

"Hakika zaka ni kwa mafakiri, masikini, wenye kuzifanyia kazi, wenye kuzoweshwa nyoyo zao, watumwa, wenye madeni, katika njia ya Allah, na aliyekatikiwa na safari, ni faradhi hiyo kutoka kwa Allah na Allah ni mjuzi mwenye hekima".

Na haichukuliwi (*ushr)* isipokuwa kutoka kwa nafaka aina nne.

Ametoa Hakim, Baihaqy na Tabarani kutoka kwa Hadithi ya Abi Musa na Muadh wakati Mtume (SAAW) alipowatuma Yemen kuwafundisha watu jambo la dini yao, akasema:

Inaendelea uk 8

Uzuri wa mwanamke katika nchi za Magharibi na dunia kwa upana unafahamika kwa mtazamo maalumu, hufafanuliwa ati mwanamke awe mrefu, mwenye umbo mwanana, na sifa linganifu kwa uzuri wa sura, pua ya wastani, midomo ya kuvutia na nywele nyepesi zenye mremeto mara nyingi hupendelewa ziwe ndefu.

Kipimo hiki cha *'mwanamke mzuri'* kimefafanuliwa na mataifa ya Magharibi ya kibepari ambapo mwanamke anayefikia kipimo hicho huhusishwa na ufanisi, kujiamini, na thamani ya kuheshimiwa katika jamii. Germaine Greer, Mwandishi na Mtetezi wa Haki za Wanawake wa Magharibi anaelezea uhusiano kati ya uzuri na mafanikio katika kitabu chake kinachoitwa 'The Whole Woman' kwa kusema:*''Kila mwanamke anajua kwamba, licha ya kupata mafanikio mengine yote, atakuwa amefeli kama yeye si mzuri''*

Kwa bahati mbaya wanawake wa Kiislamu nao pia wamekumbwa na fikra hizi chafu na janga hili la kujitumbukiza katika fani ya urembo ili nao ati wapate thamani katika jamii.
Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba mtazamo huu anaotaka mwanamke kushikamana nao si tu unawakilisha mwanamke namna anavyotaka kujionesha kiwiliwili chake kwa ulimwengu. Lakini pia



unawakilisha haiba yake halisi, jinsi anavyoyachukulia maisha na jinsi anavyotaka kuishi maisha hayo.
Mwanamke wa kiMagharibi hujivuna kwa kuwa yuko imara na huru mwenye kujitegemea, anashikilia imani kuwa yupo huru kufanya anavyotaka na kuishi maisha anayotaka - kama yalivyo madai ya jamii zote huria za kidemokrasia. (secular liberal). Lakini ukweli uko mbali kabisa na mtazamo huu wa kijahilia. Jamii ya Kimagharibi ya kibepari ambayo inajali zaidi maslahi kuliko misingi ya utu ndio iliyoweka kipimo cha mambo gani yanayofanya 'uzuri' ukamilike, na kwa sababu ya mtazamo huu huwafanya wanawake ni wenye kupagawa katika mambo ya mitindo na majarida ya urembo bila ya kutaja matumizi ya mabilioni kwa mambo ya urembo na nyengine kwenda kwa fani ya urembo wa mwili na viwanda vya vipodozi.

Je kipimo cha urembo cha ki Magharibi kinaweza kupatikana?

Mafanikio ya masuala ya urembo na viwanda vya vipodozi vinategemea kwa kiasi kikubwa juu ya ukweli usiofichika kwamba urembo wa mwanamke mzuri kamwe haufikiwi. Kwa kuwa viwanda vinafaidika kwa wanawake kutokana na kutotosheka na maumbile yao na kuwalazimisha kugharamika kununua kila vikorombwezo/ bidhaa vya urembo au hata kufanyiwa operesheni ya urembo ili kukabiliana na mashindano ya vigezo vya urembo unaokubalika.

kutotosheka na maumbile yao na kuwalazimisha kugharamika kununua kila vikorombwezo/ bidhaa vya urembo au hata kufanyiwa operesheni ya urembo ili kukabiliana na mashindano ya vigezo vya urembo unaokubalika.

Kwa hakika, haingii akilini kutarajia kuwa mwanamke wa jamii moja achilia mbali dunia nzima, apimwe kwa urefu fulani, uzito fulani, rangi fulani ya mwili na nywele, kwa sura fulani na umri fulani. Ukweli ni kwamba fikra hii haiendani na hali halisi ya maisha. Bali kinachojitokeza zaidi katika hili ni sekta ya matangazo ya mara kwa mara ili kupima kwa vipimo bandia kama vile picha za warembo, na matumizi ya teknologia ya elektroniki ili kuchapua kipimo cha haiba ya mrembo bora.

Katika Uislamu hakuna dhana potofu ya kimagharibi juu ya urembo. Uislamu haujishughulishi kabisa kuweka viwango vya udanganyifu na visivyowezekana vya urembo, kisha kutarajia kuvifikia, badala yake umetuwekea ipi picha halisi tunahitaji kuwa nayo katika mazingira mbalimbali. Uzuri kwa mwanamke wa Kiislamu ni kufuata hukmu za

Inaendelea uk 6

Chuki dhidi ya Wageni nchini Kenya unaibua maswali kuhusu jumuiya hizi za kikanda kuwa zina maana gani hasa. Ni wazi kwamba mashirika yote haya si kitu bali ni mikusanyiko ya kupiga soga, kupoteza muda na nyenzo za kikoloni.

Uislamu chini ya Serikali yake ya Khilafah utawahudumia wananchi wake kwa umakini mkubwa kwani ina wajibu wa kufanya hivyo kutoka kwa Muumba. Kwa maneno mengine, Khilafah kamwe haitotumia visingizio vya urongo kama chuki na ubaguzi wa wageni ili kukimbia wajibu wake. Zaidi ya yote, Zadi ya yote Uislamu iko mbali na aina zote za chuki na ubaguzi, iwe ni chuki na ubaguzi dhidi ya Wageni, ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa Kidini, ubaguzi wa Lugha, ubaguzi wa Kikabila nk.

Allah Taala Anasema katika Qur'an Tukufu:

"Enyi mlioamini! Hakika tumewaumbeni kutokana na mwanaume mmoja na mwanamke mmoja na tumewajaalia mapote na makabila mbalimbali ili muweze kujuana…" [TMQ 49:13].

Imeandikwa na Said Bitomwa

Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania

Kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

****

kisharia, na ubaya ni kuziwacha hukmu hizo na kufuata matamanio ya nafsi zetu.

Kushikamana na aina hii ya muelekeo ni kitu ambacho kimo ndani ya uwezo wa kila mtu, na Uislamu unatukomboa kutoka katika shinikizo kuwa 'ndani ya mbio za urembo' na kubadilisha ngozi zetu, upana wa umbo letu nk. Mambo ambayo udhati wake hayakubaliani na hali halisi na hayawezekani kamwe.

Mwanamke wa Kiislamu ana msingi madhubuti wa kujihukumu yeye mwenyewe na wengine. Msingi huu haubadiliki kulingana na kufuata kila mkondo unaoibuka. Yeye anachojali ni juu ya utii kwa Mwenyezi Mungu na ana uhakika kuwa hiki ndicho kipimo sahihi cha mafanikio.

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ (الحجرات:

"Hakika Mbora wenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu miongoni mwenu.
(TMQ 49: 13)

Kwa hivyo, suala kubwa tunalopaswa kuwa nalo si urembo wa 'ndani' au urembo wa 'nje' lakini cha msingi ni kuwa kitambulisho/ shakhsiya kamilifu ya Kiislamu. Shakhsia ambayo inayabeba mambo yote ndani ya mipaka ya Uislamu pekee.

Aidha, tunapaswa kutambua kwamba kuna udanganyifu wa mabilioni ya pesa unaoendelea. Hakuna mwanaadamu wa kweli anayeonekana kama picha zilizo ndani ya majarida ya warembo, ambazo daima hughushiwa na za udanganyifu. Maadili tunayopaswa kushikamana nayo lazima yawe ni kutoka ndani ya Uislamu peke yake, kwa kuwa huu ndio mtazamo sahihi kwa kila kitu.

Hebu tuweni wanawake Waislamu wanaofikiri ambao hujali vitu sahihi na sio kuburuzwa na yale wanayovaa wanaoitwa wanamitindo na warembo maarufu. Ambapo vipodozi kutufanya sisi wanawake kuonekana weupe, na upumbavu wa chakula gani cha kujaribu kesho ili kufinyanga miili yetu.

Mwisho wa maneno mfumo unaotawala dunia ni wa kibepari, haujali zaidi ya utajirisho wa mapesa, na hiyo ndio sababu ya msingi inayowafanya kuweka vipimo hivi ambavyo ni wajibu kuvipinga kwa nguvu zote na kuleta mabadiliko.

***Dr. Sarah Siddiqui* kitaaluma ni daktari pia ni Mchambuzi wa Kujitegemea wa Kisiasa, anaishi Karachi, Pakistan.**

****

BAADHI YAMATUKIO YA MWEZI NOVEMBA

2/11 1917 – Uingereza chini ya Waziri wake wa Nje, Arthur James Balfour yatangaza kuunga mkono kuasisiwa dola ya Mayahudi ndani ya Palestina. Tamko rasmi la Waziri Balfour (The Balfour Declaration).

2/11/1844 – Kuzaliwa Khalifa Mehmed V. Alifariki mwaka 1918.

Makala hii inakusudia kufafanua ni mambo gani Waislamu wanaruhusiwa kisheria kuchukua kutoka kwa makafiri, yaani katika matumizi yao ya kila siku, na mambo gani Waislamu hawaruhusiwi kuiga au kuchukuwa kutoka kwa makafiri.

Sababu iliyotusukuma kuandika mada hii ni kuwa Umma wa Kiislamu umepata bahati mbaya ya kusibiwa na vita vya kifikra kutoka kwa makafiri wa kimagharibi hali iliyopelekea kuchanganyikiwa katika kuchukuwa msimamo juu ya mambo yanayotokana na wamagharibi.

Katika kuchanganyikiwa huku kukapatikana makundi mawili yaliyokwenda kombo na mbali (extreme) :

Kundi la kwanza likapiga marufuku kuchukuwa kila kitu kutoka kwa makafiri. Wakakataa fikra zao na thaqafa yao kama itikadi ya wamagharibi ya kuitenga dini kando maisha kando (hii kwao ni imani kamili na si msemo tu wa kawaida), na pia wakapinga kila kitu hata vitu vya kawaida vya kimatumizi vya kimada kama vile simu, redio, tv, magari na hata mazulia ya misikitini.

Kundi la pili wao wakakubali kila kitu, na kuona hakuna tatizo kuchukuwa na kuiga chochote kutoka kwa makafiri. Basi kundi hili wakaruhusu yote yatokayo kwa makafiri kuanzia vitu vyao vya ugunduzi wa kisayansi kama simu, computer, na mashine zote. Pia wakabeba na fikra zao, mitazamo yao juu ya maisha,



juu ya mwanamke, siasa, jamii, elimu ya uchumi, utawala nk. Na mpaka ikafikia kiwango kundi hili halioni hata tabu kutawaliwa au kutawalisha fikra na sheria za kikafiri au kuzipigia debe fikra za kimagharibi. Na wengine kuthubutu kuwa majasusi wa serikali hizi za kikafiri, na wanapoonywa juu ya uharamu wa jambo hili, majibu yao huwa mbona na wewe unatumia simu, kamera na magari ya makafiri?

Ni wazi kuna utata ambao lazima ufunguliwe ili Waislamu wenye ikhlasi waweze kujua lipi linajuzu kuchukua kutoka kwa makafiri na lipi halijuzu.

Hivyo, hakuna budi kuweka kanuni fafanuzi yenye kumpa kipimo thabiti kila Muislamu kuweza kujua jambo lipi linafaa kuchukua kutoka kwa makafiri na jambo lipi ni haramu kulibeba.

Na kanuni yenyewe inaanza kwa kuwa bila ya kikomo (mutlaq) na kisha inakuja kwa kuwepo kikomo (muqayyad)
Kwa upande wa bila ya kikomo (mutlaq), ni haramu kuchukuwa kutoka kwa makafiri kila aina ya fikra (hadhara). Na ni halali kuchukua kutoka kwa makafiri kila aina ya vitu vya kushikika (madaniyah)

Yaani ni haramu Waislamu kuiga mawazo na fikra za makafiri zenye kuambatana na itikadi zao, mila zao, thaqafa zao nk. Mfano fikra za 'uhuru' zenye kumfanya binadamu kuwa huru pasi na mipaka ya kisheria mpaka wakapatikana mashoga, wasagaji, watembea uchi na wanamiziki nk. Au kumpa nafasi binadamu ya kutunga sheria kupitia mabunge na mabaraza ya wawakilishi, na hali jambo hili kwa itikadi ya Kiislamu ni haramu, bali ni kufru kamwe. Pia ubaguzi na aina zake zote (utaifa, urangi, umajimbo, ukabila nk.) au kupigania haki za wanawake zenye kuwatovua adabu kwa waume zao na wazazi wao, usawa wa kijinsia, haki za watoto zinazowafanya watoto wasiwe na huruma wala adabu kwa wazazi wao na mfano wa hayo.

Na ni halali Waislamu kuiga katika kutengeza na kuchukua kwa matumizi vitu vya kushikika(madaniyyah) ambavyo si fikra wala mawazo. Kwa lugha nyingine vitu vya kiwandani kama magari, pikipiki, simu, computer, meli, ndege, tv nk.

Amma kwa upande wenye kikomo (muqqayad) itakuwa ni halali kuchukua fikra na mawazo yao ambayo hayana uhusiano na itikadi zao, mila zao, au thaqafa zao. Kama somo la hesabu, masuala ya mbinu za uendeshaji mambo, usimamizi wa shughuli, na masomo ya namna ya upangaji wa biashara, mbinu za kiuchumi katika ukuzaji, uzalishaji viwandani, namna ya kutafuta masoko na yanayofanana hayo.

Kwa hakika haya kiasili ni fikra na mawazo lakini hayana

Inaendelea uk 8

Tunayokatazwa kutoka kwaMakafiri ..kutoka uk 7

uhusiano wowote na mila zao au itikadi zao. Bali ni mawazo yaliyo kando na mila zao, nayo ni matokeo ya ubunifu tu.

Aidha, itakuwa ni haramu kuchukua au kuiga hata kitu cha kushikika (madaniyah) ambacho kina uhusiano na itikadi zao, mila zao na thaqafa zao. Kama vile msalaba, masanduku ya kusafirishia maiti, mavazi ya makasisi na mapadri au vazi lenye alama iliyothibitika kuwa ya freemason (iwe hakika na si kwa maneno ya mitaani tu) kengele za makanisani, vazi la taifa nk.

Vitu hivi japo asili ni vya kimadaniya/vyenye kushikika na sio vya fikra lakini vinawakilisha hadhara/fikra na mila zao. Basi itakuwa ni haramu kwa Waislamu kuvichukuwa kwa matumizi yao.

Anasema Sheikh Abuu Iyaasi:

"Kufuata mambo ya makafiri ni pande mbili: Kuna kuwafuata makafiri katika mambo ya dini, na kuna kuwafuata makafiri katika mambo ya kidunia. Basi itakapokuwa kuwafuata huko ni katika vitendo vyao na mambo yao yenye fungamano na dini yao, basi kufuata huko kutakuwa ni kuwafuata katika mambo ya dini. Na itakapokuwa kuwafuata makafiri katika vitendo vyao na mambo yao yasiyokuwa na fungamano na dini yao, kuwafuata huko ni kuwafuata katika mambo ya kidunia. Amma kuwafuata makafiri katika mambo ya dini ni haramu na kujiepusha ni wajib. Amma kuwafuata makafiri katika mambo ya kidunia si haramu wala hakuna dhambi ndani yake." (Kitabu cha Jaami-u l-ahkaam-Swalat)

Huu ndio ufafanuzi wa lipi linafaa Waislamu kuiga kutoka kwa makafiri na lipi halifai, na pia aya iliyotukataza kufuata mila za mayahudi na manasara inafahamika kwa kanuni hiyo iliyokwishatangulia. Kwani tuna fahamu wazi kuwa Mtume Swala llahu alai wasallama alipambana na makafiri wakiwemo mayahudi na manasara lakini muda huo huo hatuoni mahala popote Mtume SAAW kukataa vitu vyao, bali kuna hadithi chungu nzima zinazoonesha kuwa alikuwa akitumia vitu vyao kama mikuki, pinde, panga, nguo nk.

Kwa hivyo, baadhi ya Waislamu huchanganyikiwa na kukubali fikra za kikafiri zote, na baadhi kupinga zote hata vitu vya kimatumizi kama tv, redio, simu nk. Japo upingaji wao unawasuta kwani vitu hivi wanavitumia. Na baadhi hukataa pale wanapoambia demokrasia ni ukafiri kwa kuleta hoja za kwanini tunatumia magari, simu, mashine, pesa zao?

Hitimisho

Hadhara ni mkusanyiko wa fahamu jumla juu ya maisha (vipi mfumo fulani unavyoamini na unavyoyachukulia). Amma madaniya ni vitu vinavyotumiwa katika kurahisisha maisha yaani vitu vya kushikika/mada au vya kutengeneza kutokana na ubunifu wa sayansi ambavyo haviwakilishi itikadi yoyote, navyo ni kwa matumizi ya watu wote. Basi hadhara itakuwa ni maalumu kwa watu fulani, dini fulani au mfumo fulani. Ilhali madaniya ni kwa watu wote bila ya kuzingatia au kuangalia dini zao, mila au mfumo. Kwani madaniya haiwakilishi imani ya dini, itikadi, wala mila ya jamii fulani.

Shingo ya ardhi ….kutoka uk 7

« لَا تَأْخُذَا الصَّدَقَةَ إِلَّا مِنْ هَذِهِ الْأَرْبَعَةِ: الشَّعِيرِ، وَالْحِنْطَةِ، وَالزَّبِيبِ، وَالتَّمْرِ»

"Musichukuwe zaka isipokuwa katika hivi vinne: ngano (sha'iir /barley), hintwa (pia ni aina ya ngano/wheat), zabibu na tende"

Ama *kharaj* juu ya ardhi, ni serikali huchukuwa kiwango maalumu kutoka kwa mwenye ile ardhi, serikali hukikadiria na hukiwekea kiwango hicho maalumu kulingana na kinacho zalishwa na ardhi kwa makadirio ya kikawaida na sio kinachozalishwa kivitendo hasa (*al-fi'iliy).*

Na hukadiriwa ile ardhi kwa kiasi inavyohimili ili asidhulumiwe mwenye ardhi wala Baitul mal. Na *kharaj* hutolewa na mwenye ardhi kila mwaka… (Umar bin Al-Khatab alimpeleka Uthman bin Haniif huko Sawad (Iraq) na akamuamrisha aipime, akaweka *diham* na *kafiiz* kwa kila *jariib* iliyoamirishwa au yenye maji na itafanywa mfano huo huo. (Ameitoa Abu Yusuf katika kitabu cha *Al-kharaj* kutoka kwa Amr bin Maimuun na Haritha bin Mudhrib). Na *kharaj* huwekwa katika hazina ya dola lakini si katika mlango wa zaka, na hutumiwa kwa njia zote inazoziona serikali zinafaa kama zinavyotumiwa mali nyengine za dola.

Allah ndie Mjuzi

Ndugu yenu Atta Ibn Khalil Abu Al-Rashtah

Amiri wa Hizb ut Tahrir